JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KILIMO

TUME YA TAIFA YA UMWAGILIAJI

# MWONGOZO WA UCHIMBAJI WA VISIMA VYA UMWAGILIAJI

JUNI, 2025

Kikuyu Kusini, S.L.P 146, Dodoma, Simu: +255 26 2962073, Barua pepe: info@nirc.go.tz, Tovuti: www.nirc.go.tz

## 1. UTANGULIZI

Mwongozo huu umeandaliwa kwa ajili ya kusaidia uendeshaji na usimamizi madhubuti wa shughuli za uchimbaji wa visima virefu kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji nchini Tanzania. Shughuli hii inatekelezwa na **Tume ya Taifa ya Umwagiliaji** kwa kushirikiana na Halmashauri, Taasisi za utafiti, Sekta binafsi, Wakulima na Wadau wa maendeleo.
Muongozo huu umeainisha Malengo, Vigezo, huduma zitakazotolewa pamoja na gharama kwa vikundi vya wakulima wadogo na wakulima binafsi.

## 2. MALENGO YA MWONGOZO

i. Kuweka utaratibu, viwango, na majukumu kwa wadau wote wanaohusika.
ii. Kusimamia matumizi na matunzo ya mitambo ya uchimbaji visima inayomilikiwa na Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji.
iii. Kuongoza utekelezaji wa huduma za uchimbaji wa visima kwa misingi ya kijamii na kibiashara.
iv. Kuhakikisha uendelevu wa miundombinu na huduma ya umwagiliaji.

## 3. VIKUNDI VYA WAKULIMA WADOGO

### 3.1 Vigezo vya kuchimbiwa kisima

Kulingana na mwongozo huu, maeneo yatakayochimbwa visima lazima yazingatie vigezo vifuatavyo: -

i. Uwepo wa shamba lisilopungua ukubwa wa ekari **40**.
ii. Uwepo wa wakulima wasiopungua **16** kwenye eneo moja.
iii. Eneo liwe katika mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa ajili ya shughuli za kilimo.
iv. Eneo liwe na shughuli za kilimo zinazofanyika na zenye uwezekano wa kuendelezwa.
v. Eneo lisiwe na mgogoro wowote.
vi. Mazao yanayohusika ni nafaka na mbogamboga.
vii. Utayari wa wakulima/wanufaika kusajiliwa na kuchangia ada ya huduma ya Umwagiliaji (kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji Na. 05).

### 3.2 Huduma zitakazotolewa kwa wanufaika

i. Upimaji wa mashamba na usanifu
ii. Utafiti na upimaji wa eneo la uchimbaji wa kisima.
iii. Kuchimbiwa kisima chenye urefu usiozidi mita 250,
iv. Kuweka mabomba yenye kipenyo cha inchi 6 hadi 8 kulingana na upatikanaji wa maji.
v. Kufungiwa mfumo mkuu wa upelekaji maji shambani ikiwemo pampu ya kusukuma maji, ujenzi wa kitako cha kuwekea tangi, ununuzi na uwekaji wa Tangi la maji

lenye uwezo wa kuhifadhi lita 10,000 na bomba la inchi 3 kwa urefu usiozidi mita 30 la kufikisha maji shambani.

vi. Uwekaji wa nishati kwa ajili ya uendeshaji wa pampu.

### 3.3 Gharama ya uchimbaji wa kisima

Wakulima watapata huduma hii kwa ruzuku ya asilimia 100% inayotolewa na Serikali.Wakulima watakaonufaika na huduma hii watakuwa katika vikundi vinavyotambulika na ofisi za Halmashauri husika.

**Jedwali 1: Gharama za Uchangiaji**

| Kundi | Gharama za Uchangiaji | Masharti kwa wanufaika |
|---|---|---|
| Kundi A: Vikundi vya wakulima wadogo | 0% | i. Kikundi kiwe tayari kusajiliwa Tume ya Umwagiliaji<br>ii. Kikundi kiwe tayari kulipia ada ya Huduma za Umwagiliaji<br>iii. Wakulima watapata huduma hii kwa ruzuku ya asilimia 100%<br>iv. Wakulima watasambaza maji katika mashamba yao |

**Zingatio:** Kila kundi litawekewa mfumo mahsusi wa uchangiaji wa Ada ya Huduma ya Umwagiliaji kulingana na aina ya mazao yanayolimwa. Mfumo huu utaendeshwa kwa mikataba ya huduma itakayohuishwa mara kwa mara ili kuhakikisha uwazi, uendelevu na ushiriki wa wakulima.

## 4. WAKULIMA BINAFSI

### 4.1 Vigezo vya kuchimbiwa kisima

i. Uwepo wa shamba lisilopungua ukubwa wa ekari 10.
ii. Eneo liwe katika mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa ajili ya shughuli za kilimo.
iii. Eneo liwe na shughuli za kilimo zinazofanyika na zenye uwezekano wa kuendelezwa.
iv. Uhalali wa umiliki wa shamba.
v. Eneo lisiwe na mgogoro wowote.
vi. Mazao yanayohusika ni nafaka na mbogamboga.
vii. Utayari wa mkulima/mnufaika kusajiliwa na kuchangia ada ya huduma ya Umwagiliaji (kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji Na. 05).

### 4.2 Huduma zitakazotolewa kwa wanufaika

i. Utafiti na upimaji wa eneo la uchimbaji wa kisima.
ii. Uchimbaji wa kisima chenye urefu usiozidi mita 250,
iii. Uwekaji wa bomba lenye kipenyo cha inchi 6 hadi 8 kulingana na upatikanaji wa maji.

### 4.3 Gharama ya uchimbaji wa kisima

Gharama za uchimbaji wa visima kwa kutumia mitambo ya Serikali itakuwa asilimia 20 (20%) pungufu ya bei ya soko kwa wakati husika.

Gharama za uchimbaji wa kisima zinajumuisha; -

i. Utafiti wa maji shilingi 1,500,000
ii. Uchimbaji shilingi 120,000 kwa mita moja kwa kutumia kipenyo cha inchi 6 ikijumuisha *pump testing*
iii. Uchimbaji Shilingi 300,000 kwa mita kwa kutumia kipenyo cha inchi 7 ikijumuisha *pump testing*
iv. Upimaji wa shamba na ufungaji wa miundombinu ya umwagiliaji utagharamiwa na mkulima
v. Gharama za upelekaji wa mtambo zitategemea umbali wa shamba

**Gharama hizi zitapunguzwa kwa asilimia 20 (20%) kama ruzuku ya serikali.** Upimaji wa ubora wa maji utagharamiwa na mkulima.

**Jedwali 2: Gharama za Uchangiaji**

| Kundi | Gharama za Uchangiaji | Masharti kwa wanufaika |
|---|---|---|
| Kundi B: Wakulima Binafsi | 100% | i. Ukubwa wa Shamba lenye ekari 10 au zaidi<br>ii. Uthibitisho wa umiliki wa shamba<br>iii. Awe na uwezo wa kulipia gharama za uchimbaji kabla ya huduma ya uchimbaji kutolewa. |

## 5. UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI

Waombaji wote wanapaswa kutuma maombi yao kwa kujaza fomu maalum inayopatikana katika ofisi za Tume ya Taifa ya Umwagiliaji wilaya, mikoa, makao makuu, na kwenye tovuti ya Tume (www.nirc.go.tz).

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kupitia;

Mkurugenzi Mkuu,
Tume ya Taifa ya Umwagiliaji,
S.L.P 146 Dodoma.
Barua pepe: info@nirc.go.tz
Kwa maelezo zaidi piga simu: **0652956444** au **0757 973617**